

JINA.....NAMBA YAKO.....

102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
(LUGHA)
JULAI /AGOSTI 2014

MUDA: SAA 2 ½

KAMUKUNJI DISTRICT KCSE EVALUATION TEST 2014

KISWAHILI
KARATASI 2
LUGHA
JULAI /AGOSTI 2014
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1. JIBU MASWALI YOTE
2. MAJIBU YAKO YAANDIKWE KATIKA NAFASI ZILIZOACHWA KATIKA KIJITABU HIKI CHA MASWALI.

KWA MTAHINI PEKEE

	SWALI	UPEO	ALAMA
1.	Ufahamu	15	
2.	Ufupisho	15	
3.	Lugha	40	
4.	I simu-Jamii	10	
	JUMLA		

SEHEMU A: UFAHAMU

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo

Halmashauri ya mpwito nchini imetoa mwongozo kuhusu majukumu yanayofaa kutekelezwa na serikali za kaunti kote nchini kuanzia Julai mwaka huu. Mwongozo huo utasaidia kuondoa wasiwasi ambao baadhi ya mashirika yasiyo ya serikali yalielezea kuwa huenda baadhi ya sekta zisipate ufadhili kutokana na utata kuhusu ni serikali ipi inafaa kuzishughulikia.

Shughuli hizi zinajumuisha kilimo ambapo zitahakikisha maendeleo ya mimea, mifugo na uvuvi. Serikali za kaunti pia zitashughulikia huduma za afya kuhakikisha kuna dawa na vifaa vya kutosha katika zahanati na hospitali. Uhifadhi wa mazingira na tamaduni za kijamii kama vile makavazi, maktaba na majumba ya burudani vilevile zitakuwa chini ya usimamizi wa kaunti.

Serikali hizo pia zitasimamia masuala ya uchukuzi kwa kushughulikia ukarabati wa barabara, taa za kudhibiti msongamano wa magari na bandari. Kulingana na taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari, serikali hizo pia zitashughulikia maendeleo ya biashara na vyama vya ushirika. "Serikali za kaunti zitajihusisha na kudhibiti mipaka na matumizi ya kawi, elimu ya chekechea na vyuo vya ufundi katika ngazi za vijijini, taarifa hiyo ilisema.

Halmashauri hiyo ilisema kuwa serikali hizo zitasimamia uhifadhi wa misitu, ardhi, huduma za maji kupambana na mikasa ya moto, dawa za kulevya na picha za ngono. Taarifa hiyo iliyotiwa sahihi na mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpwito ilisema pia serikali za kaunti zinapaswa kuhakikisha kuwa umma umeshirikishwa katika usimamizi wa raslimali za vijiji. Kulingana na kipengee cha 15 cha katiba ya Kenya, bunge la kitaifa katika muda usiopita miaka mitatu kutoka siku ya uchaguzi linahitajika kuunda sheria za kuhakikisha kuwa serikali za kaunti zimepata uwezo wa kuendeleza shughuli zake. Aidha kipengee cha 23 kuhusu ugatuzi kinahitaji Halmashauri ya Mpwito kutambua shughuli zitakazotengewa serikali za kaunti kutoka serikali kuu punde tu baada ya uchaguzi mkuu. Shughuli hizi zilitayarishwa kupitia hati ya sheria nambari 16 ya 2013.

Katiba katika kipengee cha 24 inatoa masharti ya kufuatwa kabla serikali za kaunti kuanza rasmi shughuli zake za kutoa huduma kwa wananchi.

MASWALI

(i) Yape makala haya kichwa mwafaka. (alama 1)

.....

(ii) Je, kaunti inawajibikaje katika kuwahudumia wananchi? (alama 2)

.....

.....

.....

.....

(iii) Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea Kutokana na mapuuza ya mwanadamu? (alama 3)

.....

.....

.....

(iv) Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya Kaunti? (alama 2)

.....

.....

(v) Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini? (alama 3)

.....
.....
.....
.....
.....
(vi) Ni kwa njia gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nchi kuinua kiwango cha maisha ili kufika ruwaza ya 2030. (alama 2)

.....
.....
(vii) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika Ufahamu.

(a) Uchukuzi.....

(b)Ugatuzi.....

SEHEMU B: UFUPISHO

Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana. Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza kustahiwa na kusadikikika katika mambo, shughuli na hali tofauti tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii. Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa vijulanga wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo nyeti ya maisha yao.

Kwa hivyo, ni dhahiri shahiri kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya kdi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, mathalani jukumu ama dhima Fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadilifu daima atajiepusha na shutuma na majanja yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemu maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu, kwamba "aliye kando haangukiwi na mti." Pia waliambiwa kwamba, pilipili usiyoila yakuwashiani?

Ni bayana kutokana na misemo hiyo mwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuwakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya 'watoro' ambao ni watovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wako mazingirani mwake. Ndipo wa kale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.

Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake. Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.

Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani, watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu. Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

(a) Nini umuhimu wa nidhamu? (maneno kati ya 50-55)
(alama 1 ya mtiririko) (alama 6)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (tumia Maneno 55-60) (alama 1 mtiririko) (alama 7)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Bainisha sifa zinazotofautisha sauti zifuatazo. (alama 2)

/e/ na /u/

(b) (i) Ainisha viambishi tamati katika neno lifuatalo. (alama 1)

Aliwalilia

(ii) Eleza maana ya mzizi. (alama 1)

(c) Pigia mstari silabi inayowekwa shadda katika neno lifuatalo. (alama 1)

Alituchochea

(d) Eleza matumizi matatu ya kiimbo. (alama 3)

(e) Tunga sentensi moja ukitumia kiwakilishi kisisitizi cha karibu
Katika ngeli ya LI- YA umoja (alama 2)

(f) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigiwa
Mstari kuwa nomino.
Mama alituambia hadi tukafurahi. (alama 2)

(g) Ainisha vitenzi katika utungo ufuatao. (alama2)
Huyu alikuwa angali bwenini.

(h) Ainisha vivumishi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mtoto wa jirani ana shamba kubwa.

(i) Tambua na ueleze aina za vihusishi. (alama2)

Mti ulioanguka karibu na darasa utachomwa hadi uishe.

(j) Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo (alama 1)

Mwalimu mnene zaidi anamiliki shamba lile kubwa.

(k) Andika neno lenye silabi mwambatano (alama 1)

(l) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya: (alama 3)

(i) Nukta mbili

(ii) Kibainishi

(iii) Kistari kifupi

(m) Tambua aina ya virai katika sentensi zifuatazo: (alama 2)

(i) Uzembe ni adui wa maendeleo.

(ii) Paka alikuwa amejificha chini ya kitanda.

(n) Andika katika hali ya mazoea: (alama 2)

Mtambo ambao unakarabatiwa leo utatufaa.

(o) Tambua aina mbalimbali za nomino katika sentensi hii. (alama2)

Kundi la wajenzi limemjengea Swaleh nyumba ya kuhifadhia Maziwa.

(p) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti ya maana kati ya (alama 2)

guna

kuna

(q) Changanua kwa kutumia mtindo wa jedwali (alama 4)

Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema walileta vyakula
Vingi sana.

(r) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)

“Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba
radhi?” Phanice aliuliza.

(s) Tunga sentensi ukitumia kitenzi chenye asili ya kigeni. (alama 1)

(t) Andika sentensi hii katika hali ulizopewa.

Nyumba yao imevamiwa na nyoka mkubwa. (alama 2)

Udogo.....

Ukubwa.....

SEHEMU D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(I) Watu wanapozungumza huenda wakafanya makosa ya sarufi Kimatamshi na hata kutumia msamiati vibaya.

(a) Eleza sababu zozote nne za kufanya makosa haya. (alama 8)

(b) Makosa haya huathiri vipi mawasiliano.? (alama 2)